MOSHI
TANZANIA

# MANISPAA YETU

www.moshimc.go.tz | Toleo La 01 | Kitengo cha Mawasiliano | Manispaa ya Moshi




HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI MUNICIPAL COUNCIL

HALIUZWI

moshimanispaa www.moshimc.go.tz

Julai - Septemba 2022




# FEDHA ZA TOZO ZAENDELEA KUBORESHA SEKTA YA AFYA MANISPAA YA MOSHI

SERIKALI ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha sekta ya afya kupitia fedha za tozo ambapo safari hii jumla ya shilingi milioni 250 zilizotolewa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi zinatarajiwa kutumika katika kuboresha kituo cha afya cha Shirimatunda kilichopo Kata ya Shirimatunda.

Mkurugenzi wa Manispaa Ndg. Rashid Gembe amesema fedha hizi zitatumika katika upanuzi wa kituo hicho kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya Mama na Mtoto, jengo la upasuaji, njia ya kupitia wakati wa kutoa na kupata huduma (walkway) na jengo la kufulia.
"Moboresho haya yatasaidie kutoa huduma kwa karibu zaidi kwa wagonjwa ambao walikuwa wakisafiri mwendo mrefu kutoka kata ya Shirimatunda na Kata za jirani kwenda hospitali ya rufaa ya Mkoa au ile ya rufaa ya Kanda ya KCMC kufuata huduma ambazo zitapatikana baada ya maboresho ya kituo hiki", alisema.

Gembe aliendelea kusema kuwa mbali na wakazi wa kata ya Shirimatunda, Soweto na Karanga kunufaika na maboresho hayo pia wananchi walioko maeneo ya vijiji vya Shirimgungani na Mijengweni wilaya ya Hai watanufaika na maboresho hayo . Kwa mujibu wa Gembe hiyo ni awamu ya pili ya fedha kutolewa na Serikali kwa ajili ya maboresho ya kituo hicho cha Shirimatunda kufuatia jumla ya shilingi milioni 250 zilizotolewa awali ambazo alisema zilifanikisha ujenzi wa jengo la kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD) na maabara katika kituo hicho jambo ambalo alisema limewaongezea ari ya kufanya kazi wahudumu walioko kituoni hapo.

Mbali na watumishi kuridhika, maboresho haya pia yamewahamasisha wananchi na kusababisha idadi ya watu wanaopata huduma katika kituo hicho kuongeza kutoka wastani wa watu 20 na 25 kwa siku na kufikia 30 na 35 kwa siku", alisema.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi Mhandisi Zuberi Kidumo ameishukuru Serikali kwa kutoa fedha hizo za Tozo ambapo amesema kuboreshwa kwa huduma katika kituo hichi ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 lengo lake ni kutoa huduma bora na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi .

"Nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Moshi kuipogeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe . Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ilivyokuwa mstari wa mbele katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na jinsi ilivyokuwa mstari wa mbele kuboresha huduma za afya na kusogeza huduma hizo kwa wananchi.", alisema.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

## MIRADI INAYOTEKELEZWA KWA 60% FEDHA ZA JULAI - AGOST,2022

| Na | JINA LA MRADI | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Kujenga matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Chemchem | 15,000,000.00 |
| 2 | Kukamilisha ujenzi wa matundu 12 ya vyoo Shule ya Msingi Jitegemee | 6,000,000.00 |
| 3 | Kukamilisha ujenzi wa matundu 12 ya vyoo Shule ya Msingi Kaloleni ifikapo Juni, 2023 | 6,000,000.00 |
| 4 | Kukamilisha Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu Shule ya Msingi Karanga | 20,000,000.00 |
| 5 | Kukarabati darasa 1 Shule ya Msingi Karanga | 6,000,000.00 |
| 7 | Kukamilisha ukarabati wa darasa 1 na deni la fundi Shule ya Msingi Kilimanjaro | 5,000,000.00 |
| 8 | Kukamilisha ujenzi wa matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Korongoni | 2,000,000.00 |
| 9 | Kujenga matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Majengo | 15,000,000.00 |
| 10 | Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Mandela | 8,000,000.00 |
| 11 | Kukamilisha ujenzi wa matundu 12 ya vyoo Shule ya Msingi Miembeni | 6,000,000.00 |
| 12 | Kujenga darasa 1 na madawati 25 Shule ya Msingi Mnazi | 25,000,000.00 |
| 13 | Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Moshi | 20,000,000.00 |
| 14 | Kujenga matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Njoro | 15,000,000.00 |
| 15 | Kujenga matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Rau | 15,000,000.00 |
| 16 | Kukamilisha ujenzi wa matundu 18 ya vyoo Shule ya Msingi Shaurimoyo | 8,000,000.00 |
| 17 | Kujenga matundu 8 ya vyoo Shule ya Msingi Sokoine | 20,000,000.00 |
| 18 | Kukamilisha matundu 8 ya vyoo Shule ya Msingi Soweto | 5,000,000.00 |
| 18 | Kujenga darasa 1 na madawati 25 Shule ya Msingi Uhuru | 25,000,000.00 |
| 20 | Kukamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Msaranga | 150,000,000.00 |
| 21 | Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu Sekondari ya Msaranga | 45,000,000.00 |
| 22 | Kukarabati miundombinu ya Zahanati ya Kaloleni | 20,000,000.00 |
| 23 | Kujenga kichomea taka kwenye Zahanati ya Shirimatunda | 25,000,000.00 |
| 24 | Ukamilishaji wa Kata ya Mfumuni | 10,000,000.00 |
| 25 | Kufunga mfumo wa CCTV Camera jengo la utawala | 30,000,000.00 |
| 26 | Kununua Maghuba mawili (2) ya kukusanyia taka ngumu | 30,000,000.00 |
| 27 | 10% ya Wanawake Vijana na watu wenye Ulemavu | 60,507,159.05 |
| | **JUMLA** | **592,507,159.05** |



# MANISPAA YA MOSHI YAPITISHA RASIMU YA SHERIA MPYA YA UKARABATI WA MAJENGO



BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Moshi limepitisha rasimu ya Sheria Ndogo ya kuruhusu ukarabati wa Majengo kwenye maeneo ya biashara yaliyo katikati ya Mji (Central Business District).

Rasimu hiyo ya Sheria ya ukarabati ina lengo la kuweka uwazi wa jinsi ya kupata kibali cha ukarabati na kuondoa urasimu uliokuwepo hapo awali.

Akizungumza baada ya kupitishwa kwa rasimu hiyo Meya wa Manaispaa ya Moshi Mhandisi Zuberi Kidumo alisema sheria hii itasawasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kujenga ghorofa waweze kukarabati majengo yao ili yawe katika hali nzuri inayoendana na hadhi ya Manispaa ya Moshi.

“Sio siri kuna baadhi ya nyumba zilizopo katika ya Mji ni chakavu na wanaoishi kwenye nyumba hizo kwa sasa hawana uwezo wa kujenga ghorofa hivyo Halmashauri imeona kuna umuhimu wa kupitisha sheria hii ili kuwasaidia waweze kufanya ukarabati na kukaa mahali pazuri na salama”Alisema Mhandisi Zuberi

Sheria hii pia itasaidia Manispaa ya Moshi kuongeza mapato kwani kuna viwango mbalimbali vimewekwa kama ada ya kibali cha ukarabati mjini.

Naye Mwanasheria wa Manispaa ya Manispaa ya Moshi,Sifael Kulanga alisema rasimu hii ya Sheria ndogo ni ya ukarabati wa Majengo katika ya Mji na haijafuta Sheria na utaratibu wa maombi vibali vya ujenzi wala Mpango Kabambe (Master Plan) unaomtaka mmiliki wa kiwanja/jengo katikati ya Mji hasa Kata za Bondeni,Mawenzi , Kiusa na baadhi ya maeneo la Kata ya Korongoni kama mtu anataka kujenga ajenge jengo la ghorofa.



# TASAF YAENDELEA KUBADILISHA MAISHA YA WAKAZI WA MANISPAA



*Nilianza kwa kufuga bata wadogo baada ya walikua niliwauza na kupata fedha ya kuanzisha miradi midogo midogo na nilijiunga kwenye vikundi ambavyo viliniwezesha kukopa na kuanza kununua vifaa vya ujenzi na kwa sasa nimekamilisha ujenzi wa nyumba ya kuishi".*

*Hayo yanabainishwa na*
*Amina Mruma mmoja wa*
*wanufaika wa TASAF kutoka Mtaa wa Matindigani Kata ya Pasua*



Amina anapokea kiasi cha Tsh 72,000 kwenye zoezi la uhawilishaji fedha kila baada ya miezi miwili kiasi ambacho ameweza kukitumia kuanzisha miradi midogo midogo,kusomesha watoto na hatimae kujenga nyumba ya kuishi.
Anasema alianza kwa kununua bata wadogo wa tsh 30,000 na baadae walikuwa na kuuza na kupata tsh 100,000 ambazo pia alizitumia kama hisa kwenye vikoba iliyomuwezesha kukopa na kununa vifaa vya ujenzi.

•

"Kupitia mradi wa ufugaji wa bata na biashara ya genge pamoja na kukopa nilianza kununua vifaa vya ujenzi kwa awamu hadi kuweza kuanza ujenzi wa nyumba yangu ya vyumba viwili ambayo hata hivyo mpango wangu ni kuendelea na ujenzi kuwa na makazo bota"Anasema Amina.
Akielezea maisha yake kabla ya kuingia kwenye mradi wa TASAF, Amina anasema maisha yalikuwa magumu na kushindwa kumuda mlo mmoja kwa siku, huku wakiishi makazi duni,na kushindwa kulipa ada na kununua sare za shule.

"Naweza kusema TASAF imebadilisha maisha yangu kwani mambo yote nimeweza kuyafanya kupitia fedha ambazo nlikuwa nazipata ikiwemo kulipa ada na sare za watoto pamoja na kuendelea na miradi midogo midogo".
Amina anamtizamo tofauti na wanufaika wanaosema fedha wanazopewa na TASAF ni kidogo, anasema hakuna fedha ndogo inategemea na jinsi watu wanavyofikiri pamoja na matumizi sahihi ya fedha.

# MUHTASARI WA TAARIFA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**UTANGULIZI**

Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 yameandaliwa kwa kuzingatia Hali halisi ya mapato na matumizi katika bajeti ya mwaka 2020/2021, Mapitio ya mwenendo wa mapato na matumizi katika bajeti ya mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwezi Desemba 2021. Aidha,Mpango huu umezingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023, Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 hadi 2025, Vipaumbele vya Serikali na Manispaa kwa ujumla.

Vipaumbele vya Manispaa ya Moshi katika bajeti ya mwaka 2022/2023 ni:

- Kuibua vyanzo vipya na kuboresha ukusanyaji wa mapato
  Halmashauri imeongeza Bajeti ya mapato ya ndani kutoka Tsh.6,432,335,999.56 Mwaka 2021/2022 hadi kufikia Tsh. 8,544,452,000.00 Mwaka 2022/2023. Kati ya fedha hizo Tsh.5,882,353,121.00 ni mapato halisi na Tsh.2,662,098,879.00 ni mapato Fungiwa. Ongezeko hilo limetokana na:

- Vyanzo vipya vya mapato: (Ujenzi wa kiwanda cha mbolea ya Mboji na ununuzi wa Mashine ya kukoboa Mpunga na na ujenzi wa Ghala la kuhifadhia mpunga).

- Kuongezeka kwa kiwango kwa baadhi ya vyanzo vilivyopo.

  Kuingizwa kwa fedha za Marejesho ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika bajeti

- Kulipa madeni ya Serikali na Wazabuni

- Manispaa imetenga fedha kwa ajili ya kulipa kodi ya ardhi kwa majengo ya Serikali, na kulipa madeni ya wazabuni.

## 2.0 MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi inatarajia kukusanya na kupokea Jumla ya Tshs.51,093,185,000 kutokana na fedha za Mapato ya ndani, Matumizi mengineyo, Miradi ya Maendeleo na Mishahara kama inavyoonekana katika Jedwali

# MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

| | ITEM | |
|---|---|---|
| A: | **MAPATO YA NDANI** | |
| | Mapato halisi | 5,882,353,121.00 |
| | Mapato Fungiwa | 2,662,098,879.00 |
| | **Jumla mapato ya Ndani** | **8,544,452,000.00** |
| B: | **MATUMIZI MENGINEYO (OC)** | |
| | Ruzuku ya uendeshaji - Elimu | 83,811,000 |
| | Usafiri likizoni - Elimu | 200,200,000 |
| | Uhamisho - Elimu | 121,000,000 |
| | Kilimo na Mifugo | 34,902,000 |
| | Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe | 149,831,000 |
| | Miundombinu | 24,133,000 |
| | Utawala | 129,532,000 |
| | **Jumla OC** | **743,409,000** |
| C: | **MISHAHARA** | |
| | Mishahara | **32,012,839,000** |
| D | **FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO** | |
| | **Fedha za Ndani** | |
| | Ruzuku ya uendeshaji | 309,634,000 |
| | Chakula Kutwa na bweni | 1,434,645,000 |
| | Posho Waratibu, walimu wakuu na wakuu wa shule | 189,000,000 |
| | Mitihani | 542,377,000 |
| | Fidia ya Ada Kutwa na bweni | 259,710,000 |
| | Ujenzi wa jengo la Utawala | 1,000,000,000 |
| | Mradi Mkakati | 2,000,000,000 |
| | Mfuko wa Jimbo | 62,524,000 |
| | Ununuzi wa Vifaa Tiba Kwa Zahanati | 50,000,000 |
| | Ununuzi wa Vifaa Tiba Kwa Vituo vya Afya | 150,000,000 |
| | Ukamilishaji wa Hospitali za Wilaya | 500,000,000 |
| | Ukamilishaji wa Zahanati | 50,000,000 |
| | Ujenzi wa Madarasa Shule Kongwe za Msingi | 180,000,000 |
| | Ukamilishaji wa Madarasa Shule za Msingi | 50,000,000 |
| | **Jumla ndogo fedha za Ndani** | **6,777,890,000** |
| | **Fedha za Nje** | |
| | Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF) | 256,396,000 |
| | Mfuko wa Jamii (TASAF) | 632,160,000 |
| | Mradi wa Watoto chini ya miaka 5 (U5BRI) | 10,000,000 |
| | EGPAF (5429) | 140,559,000 |
| | SEQUIP | 573,000,000 |
| | Boost Primary Student Learning- EP4R | 1,290,000,000 |
| | Mradi wa kudhibiti Malaria | 2,827,000 |
| | Mradi wa kuimarisha Afya(Health System Strengthening - GAVI) | 109,653,000 |
| | **Jumla ndogo Fedha za Nje** | **3,014,595,000** |
| | **Jumla Miradi (C + D)** | **9,792,485,000** |
| | **JUMLA KUU BAJETI (A+B+C+D)** | **51,093,185,000** |



# MANISPAA YA MOSHI YAWEKA MIKAKATI YA KUIMARISHA USAFI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi imeanza mikakati ya kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuhakikisha utekelezwaji wa sheria ndogo ya usafi na Mazingira ya mwaka 2006 na Marekebisho yake ya mwaka 2019 inafuatwa ili kuendeleza sifa ya Manispaa ya Moshi ya kuwa Manispaa safi ikilinganishwa na Manispaa nyingine hapa nchini.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Ndg. Rashid Gembe ambapo amesema ili kufikia azma hiyo, uongozi wa Halmashauri utahakikisha sheria hii inatekelezwa vilivyo na ukamataji wa wachafuzi na waharibifu wa mazingira watakamatwa na kutozwa faini ya papo kwa papo isiyopungua kiasi cha Shilingi Elfu Hamsini au kifungo cha miezi sita jela.

“Sheria hii inapiga marufuku utupaji wa taka ovyo, utemaji wa makohozi, utiririshaji wa maji ovyo pamoja na kujisaidia ovyo ambapo kwa yeyote atakayetenda makosa hayo atatozwa faini ya papo kwa hapo isiyopungua Shilingi Elfu Hamsini” Alisema Gembe

Mikakakati mingine iliyowekwa ni pamoja na kuboresha mbao za matangazo ili kuelimisha jamii kuhusu usafi na utunzaji wa Mazingira sehemu mbalimbali za mji, kutoa matangazo kwa vipaza sauti kwenye masoko na kituo kikuuu cha mabasi, kupitisha gari la matangazo na kuendelea kushirikiana na vyombo vya Habari ili kuwakumbusha wakazi wa Manispaa ya Moshi wajibu wao juu ya usafi na utunzaji wa Mazingira.

Aidha alisema mikakati hiyo itahusisha pia ukusanyaji wa taka za aina mbalimbali zinazozalishwa katika mitaa yote ndani ya Manispaa na sehemu ya taka hizo zitatumika kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea kwenye Kiwanda cha mbolea cha mboji kilichoko eneo la Mtakuja kinachomilikiwa na kuendeshwa na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kushirikiana na Mji rafiki wa Tubingen uliopo chini Ujerumani.

“Hadi kufikia mwezi Agosti, mwaka huu, takwimu zinaonesha kuwa mji wa Moshi unazalisha jumla ya tani 236 za taka kila siku yakiwemo mabaki ya mboga mboga na matunda ambayo ni mali ghafi ya Kiwanda cha mboji na uzalishaji huo ni sehemu ya kuufanya mji wetu uwe safi”, alisema.

Gembe alisema nia ya mpango huo kabambe ni kuhakikisha Manispaa ya Moshi inandelea kushika nafasi yake ya kwanza katika Mashindano ya Usafi wa Mazingira yanayofanyika kila mwaka kwa uratibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii.

“Ushindi wetu wa kila mwaka kwa miaka mingi mfululizo ulikuwa chachu ya miji mingine hapa nchini kuiga mfano wetu katika kuhakikisha mji unakuwa safi ambapo Halmashauri nyingi zimefanya ziara za mafunzo kuja kujifunza jinsi tulivyofanikiwa kufanya mji wetu kuwa safi na kuwa kinara wa usafi hapa nchini”, alisema.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI



## MANUFAA YA KUTUMIA MASHINE ZA KIELECTRONIC KUKUSANYIA MAPATO(POS)

- Kwa Kutumia POS Ni Rahisi Kupata Taarifa Za Makusanyo
- Uhakika Wa Fedha Zote Zinazotozwa Kuingia Halmashauri
- Kudhibiti Wizi Wa Fedha Zinazotozwa

*Dai Risiti Kulingana Na Kiasi Cha Pesa Ulichotoa*

moshimanispaa www.moshimc.go.tz